



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MABADILIKO YA TAREHE YA UPIGAJI KURA

KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA MBUNGE WA JIMBO LA MUHAMBWE


Dar es salaam, 9 Aprili, 2021

Mnamo tarehe 27 Machi, 2021 Tume ilitangaza ratiba ya Uchaguzi mdogo katika Jimbo la Muhamwe ambapo tarehe ya uteuzi wa wagombea katika Jimbo husika ilipangwa kuwa 03 Aprili, 2021 na upigaji kura kuwa 02 Mei, 2021. Hadi hivi sasa uteuzi wa wagombea tayari umeshafanyika. Katika uteuzi huo, wagombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Alliance for Change and Transparency (ACT-WAZALEND) na Democratic Party (DP) wamekidhi vigezo na kuteuliwa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 46(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ina mamlaka ya kufuta siku ya uchaguzi iliyopangwa awali na kupanga siku nyingine endapo kuna sababu yoyote ya msingi au linapotoka tukio ambalo litazuia uchaguzi kufanyika.

Kwa msingi huo, Tume kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 46(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume imefuta siku ya kupiga kura katika Jimbo la Muhamwe iliyokuwa imepangwa hapo awali (02 Mei, 2021) na upigaji kura huo sasa utafanyika tarehe 16 Mei, 2021. Hali kadhalika, kampeni za ubunge katika Jimbo hilo zinasitishwa na zitaanza tena tarehe 1 hadi 15 Mei, 2021.

Imetolewa na:


Dkt. Wilson Maher Charles

Mkurugenzi wa Uchaguzi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI